SHINDANO LA AFROGREEN TRENDSETTERS

TANZANIA

UKURASA WA YALIOMO

1. JINSI YA KUTUMIA MUONGOZO HUU

2. UTANGULIZI
‘AfroGreen Trendsetter’ ni nini?

3. KUELEZEA WENGINE KUHUSU SHINDANO LA ‘AFROGREEN TRENDSETTER’
Kushirikisha wengine
- Shindano hili litaendeshwa vipi?
- Jamii yako itajuaje kuhusu shindano?
- Ni nini huchangia ingizo liweze (Vigezo vya kupata ushindi? (Nini kinapelekea kupata ushindi?)
- Mchakato wa ukaguzi (Mchakato wa maamuzi)
- Masharti ya shindano
- Tuzo

4. (KUELEZA SHINDANO LA) MAELEZO YA SHINDANO LA ‘PAN AFRICAN AFROGREEN TRENDSETTER’
- **Fomu ya kujiunga katika shindano la ‘Pan African Afrogreen’**
- **Orodha ya ukaguzi wa viingizo vya wasifu wa sauti**
- **Tuzo**

5. TAREHE MUHIMU

6. SHUKRANI

1. JINSI YA KUTUMIA MUONGOZO HUU

Karibuni wapendwa Mtandao wa Wanahabari Vijana Afrika!
Mwaka 2021 unaonaonekana kuwa mwaka wa kusisimua katika makabiliano na mabadiliko ya tabia nchi, na muongozo huu wa maelekezo umeundwa ili kukuelezea na kukupa ujasiri wa kuwa mshiriki muhimu katika shughuli yako kubwa mwaka huu. SHINDANO LA KIAFRIKA LA MABADILIKO YA TABIA NCHI! Hii inamaanisha nini ?

Muongozo huu una malengo makuu matatu:

1. kukusaidia kuelewa shindano hili la Kiafrika na jinsi litakavyoendeshwa
2. kukuandaa ili uweze kuhimiza/kuhamasisha vijana wengine na watu wazima katika jamii yako kufurahishwa na kuvutiwa na kuingia katika shindano; na
3. Kukupa maelezo ya kusimamia shindano katika stesheni yako ya redio.

2. UTANGULIZI

Shirika la Children's Radio Foundation (CRF) limetoa mafunzo kwa wahabari vijana katika vituo 42 vya redio katika nchi 5 za Afrika (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ivory Coast, Afrika Kusini, Tanzania na Zambia) ili kutengeneza vipindi vya redio kila wiki, pamoja na uendeshaji wa shughuli za kijamii kila mwezi, kuhusu mada za mabadiliko ya tabia nchi.

Tangu mwaka 2019, umeshughulikia mada kama vile Matumizi, Uuzaji, Mavazi na Mtindo, Sekta ya Chakula, Kilimo, Huduma za Mazingira, Usimamizi wa Taka, na zingine. Ukachukua wasikiliaji wa kipindi chako cha redio, na washiriki wa shughuli za kijamii, na kuwapitisha katika safari muhimu ya kuelewa dharura ya mabadiliko ya tabia nchi inayokabili jamii yako, nchi na ulimwengu wote. Kwa kweli tunajivunia ushawishi ambao umefanya kupitia mazungumzo haya, lakini, bado tuna safari ndefu ya kwenda. Chukua kwa mfano ukweli ufuatao:

- Afrika Kusini ndiyo nchi ya 13 inayotoa kiwango kikubwa cha gesi chafu ulimwenguni, na kubwa kabisa barani Afrika;
- Nchini Zambia, mabadiliko ya tabia nchi tayari yamekuwa na athari kubwa katika kilimo, usalama wa chakula, wanyama wa porini, misitu, maji, nishati na afya ya binadamu, na kuifanya kuwa nchi ya 34 iliyo hatarini zaidi kutokana na mabadiliko ya tabia nchi;
- Tanzania iko katika hatari kubwa ya mabadiliko ya hali ya hewa yanayohusiana na mabadiliko ya tabia nchi, kama vile: ukame na mafuriko, kwa sababu ya kiwango cha juu cha umaskini na kutegemea kilimo kwa kiwango kikubwa;
- Maliasili ya nchi ya Cote D'Ivoire inadhaniwa kuwa imepungua kwa 26% kati ya 1990 na 2014 kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi; na
- Katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2030 watu zaidi ya 60,000 hadi 80,000 wanaweza kuwa katika hatari ya kupata ugonjwa wa Malaria kwa sababu ongezeko la hali ya hewa ya joto husababisha kuongezeka kuenea kwa ugonjwa huo.

Ingawa kiwango cha Afrika cha uzalishaji wa gesi chafu ni kidogo ukilinganisha na sehemu zingine za ulimwengu, mabadiliko ya tabia nchi ni shida ya kila mtu. Vijana barani Afrika wana jukumu muhimu kwa sababu miji ya Afrika na idadi ya watu itaongezeka kwa kasi kuliko mahali pengine popote duniani katika miongo michache ijayo.

Lakini kwa madhumuni ya zana ya muongozo huu, tungependa kubadilisha mwelekeo wetu kutoka changamoto za mabadiliko ya tabia nchi ambazo umeshughulikia, na sasa kuzingatia mwelekeo wa 'AfroGreen Trendsetters' ili kushughulikia baadhi ya changamoto ambazo umetambua katika vipindi vyako vya redio na shughuli za kijamii.

JE, ‘AFROGREEN TRENDSETTER’ NI NINI?

‘AfroGreen Trendsetter’ ni mtu anayejali sana kuhusu suala la kupunguza athari mbaya za mabadiliko ya tabia nchi, na anatia bidii katika jamii yake kufanya hivyo.

Kutambua na kusherehekea hao ‘AfroGreen Trendsetter’ walio katika jamii zetu, tunakaribisha vituo vyote 42 vya redio kujiunga na kusaidia CRF katika maandalizi ya kwanza ya shindano la ‘Pan African AfroGreen’ inayohusisha vijana na watu wazima katika jamii yako.

Kutakuwa na hatua 2 katika shindano hili:

1. Shindano la ‘AfroGreen Trendsetter la mikoa; na
2. Shindano ya Pan African Trendsetter (kushirikisha nchi tofauti za Afrika)

3. KUELEZEA WENGINE KAMPENI YA KIAFRIKA YA SHINDANO LA AFROGREEN TRENDSETTER

Tunakualika utafute kijana mmoja ambaya ni **‘AfroGreen Trendsetter’** na pia mtu mzima mmoja ambaye ni **‘AfroGreen Trendsetter’** ili wawili hao wawakilishe jamii yako.

Sifa kadhaa ambazo hufanya mtu atambulike kama ‘AfroGreen Trendsetter’ ni:

- Mtu mzima na / au kijana ambaye amekuwa na tabia za kujali mazingira tangu zamani;
- Mtu mzima na / au kijana ambaye analinda mazingira kwa njia ambayo inakuza ushiriki wa jamii
- Mtu mzima na / au kijana anayeendeleza uimara, urafiki wa mazingira na usawa wa asili;
- Mtu mzima na / au kijana anayetumia kile kinachopatikana katika mazingira yake ya karibu ili kuleta matokeo mema katika harakati za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi;

- Mtu mzima na / au kijana ambaye huwafanya wengine wafurahi na kuhamasika kufanya mabadiliko, na anayewahimiza wengine kufahamu jinsi matendo yao yanavyoathiri mazingira ya ndani na kuchangia mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni;
- Mtu mzima na / au kijana anayeongoza kwa mfano wake mwema, na anayewahimiza wengine kuchukua tabia za “kijani”. Na mtu aliyefanikiwa kuunda harakati au shirika ambalo linachangia mazoea endelevu kuhusu maji au suala lingine lolote la mazingira ambalo linajali jamii yao; na
- Mtu mzima na / au kijana ambaye anakataa/kukashifu mazoea ya mashirika makubwa ambayo hutumia mbinu za biashara zenye madhara kwa mazingira, kwa mfano bishara zinazotumia plastiki ambazo haziwezi kutumika tena.

Baadhi ya mifano ya watu ambao ni AfroGreen Trendsetters inaweza kuwa:

- Mjasiriamali kijana ambaye hutengeneza bidhaa ambazo ni za asili na zinazozalishwa ndani.
- Mvuvi ambaye hutumia mbinu za uvuvi ambazo zinahakikisha samaki wa kutosha katika chanzo cha maji na anayeheshimu makazi.
- Msanii (Mwanasanaa) ambaye hukusanya takataka na kutengeneza mapambo ya kuuza kutoka kwake.
- Mwanaharakati anayehimiza serikali za mitaa na/au serikali ya kitaifa kutekeleza sera na mazoea ya mabadiliko ya tabia nchi.

Shindano hili Litaendeshwaje?

Wanajamii wanafursa ya kumpendekeza mtu mzima na / au kijana ambaye wanafikiria anawakilisha mwenendo mzuri na uhodari wa 'AfroGreen Trendsetter' katika jamii yako.

Wakati wa kupendekeza , ni muhimu wanajamii wahusishe yafuatayo:

- Jina na umri wa mteule;
- Maelezo ya kwanini wanamteua/wanampendekeza mtu huyo - hadithi ya kitu ambacho mtu huyo alifanya/ anakifanya ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, na kwa nini jamii wanahisi mtu huyo anastahili kupewa tuzo ya eneo la (JINA LA JAMII/ ENEO HIYO) AfroGreen Trendsetter **2021**;
- Maelezo ya mawasiliano ya aliyeteuliwa (aliyependekezwa) kuwa 'AfroGreen Trendsetter' au mahali ambapo anaweza kupatikana; na
- Majina ya wateule na maelezo ya mawasiliano yao.

Uteuzi unaweza kutumwa kupitia njia zozote zinazopatikana katika kituo chako cha redio.

Baadhi ya mifano ya jinsi ya kupokea majina ya wateule.

- Ujumbe wa sauti kupitia WhatsApp iliyotumwa kwa nambari ya kituo cha redio;
- Sanduku la uteuzi linaweza kuwekwa katika stesheni, ambapo wanajamii wanaweza kuingiza kipande cha karatasi kilichoandikwa majina ya wateuzi wao;
- Unaweza kutenga kipengele katika kipindi chako cha redio ambapo wasikilizaji watapiga simu na kufanya uteuzi wao; na
- Unaweza kuandaa shughuli ya kijamii, ambapo unawaalika watu kwenye ukumbi fulani kwa wakati fulani ili kuja na kufanya uteuzi wao hapo.

Unaweza kuchukua njia moja au zaidi kutoka kwenye mifano iliyo hapo juu. Chaguzi zaidi zitakuwezesha kufikia watu wengi zaidi.

Jamii yako itajuaje kuhusu shindano?

Tungependa kukuhimiza wewe, kituo chako cha redio, shule, na taasisi shirika kueneza taarifa na kuwahamasisha wengine kuingia katika shindano hili. Hizi ni hatua tunazofikiria unaweza kuchukua ili uweze kufanya hili:

- **Tumia redio**

Tengeneza jingle (wimbo mfupi) na/ au tangazo la shindano. Peana maelezo muhimu kama vile: ni nani anayeweza kuingia, tarehe ya mwisho, sheria ambazo zinatumika, jinsi ya kushiriki katika shindano na namna ya kuwasilisha. Ongea na msimamizi wa kituo kuhusu kucheza jingle na tangazo wakati wa kipindi chako na pia kwenye vipindi au matangazo mengine ya kila siku redioni.

- **Tumia mitandao ya kijamii**

Tumia ukurasa wako wa Facebook kupeana habari mtandaoni. Tuma maswali na maoni kuhusu mabadiliko ya Tabia nchi.
Tuma ujumbe kupitia WhatsApp kwa wenzio/makundi na vijana wengine.
Tuma vipengele vyako vilivyo Soundcloud vya mabadiliko ya tabia nchi kutoka kwenye kurasa zako tofauti za mitandao ya kijamii, ukitumia hashtag ya #AfroGreen kwa mabadiliko ya tabia nchi kwenye mitandao ya kijamii na uliza taasisi mshirika wachangie kueneza habari ya shindano.

- **Tumia vituo vya habari vya kijamii (community media)**

Ni vituo vipi vya habari vinavyopatikana katika jamii yako? Je, una uwezo wa kushirikisha magazeti ya jamii na/au vituo vya televisheni katika ukuzaji wa kampeni yako ili kufikia hadhira nyingine ambayo haungewafikia kwa kupitia njia ya redio tu?

- **Tumia karatasi**

Kuwa mbunifu! Tengeneza mabango yenye maelezo yote ya shindano na kuyabandika shuleni, kanisa, dukani, zahanati, duka kubwa na vilabu / maeneo ya / vya michezo - sehemu zile ambazo vijana wapo. Unapotumia karatasi, kumbuka kutumia njia ambayo haitaathiri mazingira.

- **Tumia sauti yako**

Neno la kinywa linaweza kwenda mbali. Waambie marafiki zako, familia na majirani. Waombe pia kushirikisha maelezo/taarifa hizo na wenzao! Uliza kanisani na shuleni ikiwa unaweza kutoa tangazo na pia kama utaandaa shughuli ya kijamii humo, na hakikisha umetaja shindano.

Ni nini huchangia ingilio la shindano kushinda?

- Uzuri haimaanishi ukubwa. Kama jaji, hauitaji kutafuta hadithi ile kubwa, lakini tafuta hadithi ile yenye maana na uendelevu.
- Mteule anahamasisha na kushirikisha wengine katika jamii ili kuleta mabadiliko?
- Hadithi hiyo inaonyesha changamoto na pia mafanikio ya mteule? Au ni hadithi ya mafanikio tu?
- Kiingilio kinahusiana na mabadiliko au uwezekano wa mabadiliko?
- Hadithi hiyo ilitoa uzoefu wa kibinafsi, na sio tu nadharia ya mabadiliko ya tabia nchi?
- Kiingilio kina ubora unaotambulika? Yaani, ni jambo tofauti au la kipekee?

Mchakato wa ukaguzi:

Kutakuwa na duru moja ya kuhukumu shindano la ‘AfroGreen Trendsetter’ kwa mkoa

- Waamuzi watapokea viingilio vyote vilivyopokelewa kwa muda uliopangwa na kuchagua washindi.
- Uchaguzi wa jopo la waamuzi hao ni fursa nzuri ya kutengeneza marafiki zaidi, mbali na mawimbi yako ya redio. Usipitishe zaidi ya watu watano unapo unda jopo lako la kuhukumu. Jopo la kuhukumu linaweza kutengenezwa na watu kama:
  - Mwanahabari kijana mmoja au wawili;
  - Mfanyakazi wa kituo cha redio au meneja wa kituo;
  - Mtaalam katika mambo ya mabadiliko ya tabia nchi (kwa mfano mwalimu wa jiografia, au mshiriki kutoka kwa taasisi shirika);
  - Mwanafunzi wa chuo kikuu anayesomea mada yoyote inayohusiana na mabadiliko ya tabia nchia; na
  - Mpigaji simu wa redio wa mara kwa mara ambaye kuchangia majadiliano na kutoa maoni ya busara kuhusu mada ya mabadiliko ya tabia nchi.
- Zoezi la kuchagua mshindi linaweza kufanywa katika kituo chako cha redio, shirika au shule.
- Unaweza kuamua kuandaa hafla ya kutangaza na kusherehekea mshindi wa AfroGreen Tendsetter wa mkoa, au unaweza kutangaza jina la mshindi na kutaja mshindi katika majukwaa yote ya media za kijamii.
- Wanahabari vijana hawawezi kuteua mtu yeyote.
- Wanahabari vijana pia hawawezi kuteuliwa.
- Uamuzi wa majaji ni wa mwisho na hakuna mawasiliano yoyote zaidi baadaye.
- Watu wanaweza kuteua watu wengi kadri wanavyotaka.
- Viingilio vingi kwa mtu yule yule vinaruhusiwa, hata hivyo zoezi la kuamua litaangalia machangio yake haswa, na sio idadi ya majina yaliyopokelewa.
- Shindano liko wazi kwa watu wote. Vijana wateule lazima wawe na umri wa miaka 10 - 24, na wateule wazima wawe wenye umri wa miaka 25 na zaidi.
- Washindi watajulishwa moja kwa moja. Majina yao yatarushwa kwenye vituo vyote vya redio, majukwaa ya mitandao ya kijamii ya CRF, na katika kipindi cha redio.
- . (Taasisi ya “Save the Children” itawasiliana moja kwa Moja na mshindi kwa njia ya simu)
- Kituo cha redio na CRF hawatatoa taarifa zako kwa mtu mwingine yeyote bila kupata idhini yako kwanza.

Tuzo

Kumbuka kutakuwa na washindi wawili kutoka kwa kila jamii. ‘AfroGreen Trendsetter’, yaani mmoja wa kundi la watu wazima na mwingine wa kundi la vijana.

Kila mshindi anapokea:

- Fursa ya kuwa mgeni katika kituo cha redio kwa fursa ya mahojiano ya moja kwa moja mbapo wanaweza kujionyesha wenyewe na kuhamasisha wasikilizaji kwa kushiriki hadithi yake.
- Tuzo ya pesa taslimu **Tsh 115,000 itatolewa kwa kila mshindi mmoja wa vijana na watu wazima** ya kutumia kwa mradi, mpango au mtindo wao wa maisha wa kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

4. KUTOA MAELEZO YA KAMPENI YA PAN AFRAN AFROGREEN TRENDSETTER KWAKO

Kwa kuwa sasa tayari umepata washindi wako (Kijana na mtu mzima) kutoka shindano la mkoa, unahitaji kuandaa uwasilishaji wako wa maingizo katika shindano kuu la ‘Pan African AfroGreen Trendsetter; ambayo yataamuliwa na timu ya CRF.

Jinsi ya kuandaa maingizo yako katika shindano la ‘Pan African AfroGreen Trendsetter’:

- Wape washindi wa shindano la mkoa maelezo ya kuwa utawaingiza katika shindano kuu la ‘Pan Africa’. (au waeleze washindi wote wa vijana na watu wazima wa mkoa kuwa utawaingiza kwenye shindano kuu)
- Rekodi wasifu wa sauti wa dakika 1-2 nao ili kupata hadithi zao

[VIDOKEZO VYA JINSI YA KUREKODI WASIFU YA SAUTI]

- **Sehemu ya 1 (mwanzo):**
  - Ajitambulishe na kutuambia kidogo kuhusu malezi yake (jina, umri, jamii, shule / kazi, hali ya kifamilia) .
  - Aeleze jinsi, lini na kwa nini alianzisha mradi wake, (kwa mfano mradi wa Usimamizi wa Taka).

- **Sehemu ya 2 (katikati):**
  - Afafanue wakati maalum anaoukumbuka au ambao alijua kwamba yeye anafanya kazi nzuri ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.
  - Afafanue alivyohisi wakati alipogundua matokeo/athari nzuri za jitihada yake. Atoe mifano.

- **Sehemu ya 3 (mwisho):**
  - Ashiriki ujumbe wa kutia moyo kwa Waafrika wengine.
  - Chukua picha nzuri ya kila mteule wa mkoa
  - Jaza fomu ya kuingilia na uitume kwenye anwani za barua pepe zilizoainishwa hapa chini.

- **Tuma form za kuingilia kwenye barua pepe hizi:**
    - Tanzania: pomycn@gmail.com na mycniro@gmail.com

FOMU YA USHIRIKIANO WA HABARI YA PAN AFRICAN

Maelezo muhimu yanayohitajika kwa mteule:

Jina:_____

Jina la familia/ukoo:_____

Jinsi:_____

Umri:_____

Kama ingilio lako ni la upande wa watu wazima au vijana:_____

Anwani:_____

Nambari ya Ardhi:_____

Namba ya simu ya mkononi : _____

Barua pepe :_____

Anwani mbadala:_____

Kituo cha Redio:_____

Kiungo cha SoundCloud kwa wasifu wa sauti ulioandaa kwa ingilio hili:_____

Picha ya mteule:

TAFADHALI TIA SAINI YAKO KWA KUIDHINISHA TAMKO LILIO HAPA CHINI:

Ninathibitisha kwamba kiingilio changu kilichowasilishwa kwenye shindano la PAN AFRICAN AFROGREEN TREDSETTERS ni kazi yangu mwenyewe na ya asili, na uwakilishi wa kweli wa shughuli na jitihada zangu za mabadiliko ya tabia nchi. Ninathibitisha kwamba nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na sheria za shindano.

_____

(Weka saini)

Natoa ruhusa na idhini yangu kwa CRF, kituo cha redio na taasisi ya KR Foundation kutumia jina langu, hadithi ya sauti na picha yangu kwenye mitandao yao ya kijamii iendapo nitaibuka kuwa mshindi.

_____

(Weka saini)

Orodha ya kuangalia viingizo vya wasifu wa sauti:

- Ikiwa unasimulia hadithi kuhusu mtu au watu, ulipata idhini yao?
- Wasifu wako wa sauti unahitaji kuwa wa kweli, kuhusu kitu halisi ulimwenguni. Sio kuhusu kitu ambacho umetunga.
- Umehakikisha kwamba ingizo lako la wasifu wa sauti linasikika vizuri?
- Hadithi yako inajumuisha maelezo muhimu, kama vile: ni wapi na lini ilitokea?
- Hadithi inajumuisha maoni yako, na pia maelezo ya kuunga mkono?
- Hadithi yako inaelezea shida na suluhisho pia?
- Jina lako kamili, umri, nambari ya simu ya mkononi na anwani ya nyumbani
- Ingilio lako linahitaji kuambatana na picha.

Tuzo

Mshindi mmoja wa watu wazima wa Pan African AfroGreen Trendsetter na mshindi mmoja wa Vijana Pan African AfroGreen Trendsetter watachaguliwa kama washindi wa mwisho na kila mshindi **atapata zawadi kubwa ya Tsh 1,150,000 taslimu.**

5. TAREHE MUHIMU

- **3 Mei:** Wito wa viingilio vya mikoa (huu ni wakati unapoalika jamii ili washiriki na uwape habari zote wanazohitaji)
- **Juni 11:** Tarehe ya mwisho ya viingizo vya shindano la mkoa (Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ya ushiriki wa shindano la mkoa)
- **14 Juni - 17 Juni:** Ukaguzi wa ingilio za mikoa (Ukaguzi wa maombi ya ushiriki wa shindano la mkoa)
- **18 Juni - 19 Juni:** (Kutangaza washindi wa mkoa) Washindi wa Mkoa walitangaza
- **21 Juni - 9 Julai:** Kuandaa viingilio (mchakato wa utumaji maombi kwa..) watu wazima na vijana kwenye shindano kuu ya Pan Africa
- **9 Julai:** Tarehe ya mwisho ya ingizo (ya kutuma maombi) kwa watu wazima / Vijana wa Pan Africa AfroGreen Trendsetters
- **17 Julai:** Kutangaza washindi wa vijana na watu wazima wa AfroGreen Trendsetter

6. SHUKRANI

CRF pamoja na shirika la KR Foundation tungependa kukushukuru kwa ushiriki wako na pia kwa njia zote za kufurahisha ambazo umezungumza kuhusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabia nchi.

Tunatumaini kupata ingilio lako na tuna uhakika kwamba wewe na wenzako mtatufurahisha.

Kila la heri.